# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS- TAMISEMI.
# SHULE YA SEKONDARI KALIUA

S.L. P 35,Kaliua**,**
Mkuu wa shule. **Simu Na:**+255685673588 na 0759313000
Makamu mkuu wa shule 0767650449 na 0784650449
Matron 0764570053.
Patron 0762775315.
**Barua pepe**,kaliuasec2020@gmail.com
**Blogs: Kaliuasec.blogspot.com**


Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi
.....
.....
S.L.P.....
.....

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI *KALIUA* - HALMASHAURI YA KALIUA MKOA WA TABORA MWAKA.....**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **.....** tahasusi ya ..... Shule ya Sekondari Kaliua ipo katika Mkoa wa Tabora, wilaya ya Kaliua, Tarafa ya Kaliua. Ni umbali wa Kilometa moja toka standi kuu ya mabasi ya Wilaya Kaliua barabara ya kwenda MKOA WA **KIGOMA.**

Muhula wa masomo unaanza tarehe..... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 Sare ya shule

- ***Sare ya shule kwa wasichana***

a) Sketi mbili za rangi **nyeusi**, kitambaa cha suti, sketi ziwe na marinda na urefu wa sketi unaotosha kugusana na kiatu, sketi isiwe inayobana mwili.
b) Shati mbili **nyeupe (tetroni)** za mikono**,** mirefu isiyobana mwili wako.
c) Nguo za **michezo**: T-Shirt mbili za njano zenye kora isiyo na mistari wala maandishi, tracksuti ya michezo (kwa wasichana tu) **rangi ya bluu bahari** zitakazovaliwa wakati wa michezo tu na mchakamchaka.
d) **Raba** za michezo jozi mbili**,** rangi yeyote isiyo na sori ndefu
e) Viatu vya ngozi **nyeusi** jozi mbili, vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi
f) **S**oks**i nyeupe** ndefu **(**stocking) jozi mbili au zaidi
g) Sweta rangi ya **bluu** yenye shingo ya ( V)

h) Nguo za nyumbani **haziruhusiwi kabisa**. Mavazi yanayoruhusiwa ukiwa shuleni baada ya masomo ni:

- **Sketi rangi ya khaki** (tunashauri awenazo mbili)
- **T-shirt za rangi ya njano** zenye kora, ambazo hazina maandishi (zitagongwa Nembo ya shule)
  - Hijabu kwa Waislamu inaruhusiwa, iwe ndefu **isiyofunika tumbo. ( kama hautaridhika na utaratibu huu wa shule**

**<u>tafadhali fanya maamuzi sahihi mapema ili usiharibu utaratibu)</u>**

- **Hijabu nyeupe** (Wakati wa vipindi madarasani)
- **Hijabu ya njano** ( Baada ya masomo)

➢ ***Sare ya shule kwa wavulana***

a) Suruali mbili rangi **nyeusi** zenye **malinda mawili** , upana wa kuanzia cm 15 na kuendelea inayoruhusu chupa ya soda kupita bila kukwama ,Shati mbili nyeupe (tetroni) za mikono mirefu zisizobana mwili na ziwe na urefu wa kutosha kuchomekea ndani ya suruali.
b) **Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili** vya kufunga kamba vyenye visigino vifupi
c) Soksi **nyeusi ndefu** (stocking) jozi mbili au zaidi
**d)** Sweta rangi ya **bluu** yenye shingo ya ( V)
e) Mkanda **mweusi** wa ngozi wa kuvalia suruali.
f) Nguo za **michezo** ( Bukta mbili , T-Shirt mbili za njano zisiwe na maandishi.
g) Nguo za nyumbani **haziruhusiwi kabisa**. Mavazi yanayoruhusiwa ukiwa shuleni baada ya masomo ni:
   - Suruali ya kaki yenye malinda na **upana** chini kuanzia **cm 15** na kuendelea inayoruhusu ***chupa ya soda kupita bila kukwama.***
   - T-Shirt za rangi ya njano ( zisizo na maandishi, zitagongwa Nembo ya shule)

**2.2 Ada na Michango ya shule**

**a)** Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini tu. (**70,000.00**) kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na tano (**35,000.00**) kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hii ya ada ilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba **51301100059**, katika Benki ya NMB, Jina la Akaunti ni **KALIUA SEC. SCHOOL CAPITATION ACCOUNT** ( tafadhali kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip, kumbuka kuwa hii ni Akaunti kwa ajili ya **ADA YA SHULE TU).**

**b) Michango mingine muhimu inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

i. Shilingi **20,000**/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi **6,000**/= kwa ajili ya kitambulisho cha shule na picha.
iii. Shilingi **20,000**/= kwa ajili ya taaluma.
iv. Shilingi **40,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 4**,000/=** nembo ya shule
vi. Shilingi **5,000**/= Fedha ya tahadhari (haitarejeshwa).
vii. Shilingi **5,000**/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
viii. Shilingi **20,000**/= kwa ajili ya Mitihani ya kujipima (***mock)***
ix. Shilingi **20,000 /=**kwaajili ya kutunza viumbe hai kwa wanafunzi wa PCB na CBG tu, kwa mwaka mzima.
x. Shilingi **30000/=** crush program kwa mwaka mzima.
xi. Mwanafunzi aje na kiambulisho cha bima ya afya au aje na feha taslimu tsh.50400 ili akatiwe bima na watoa huduma wa BIMA ya afya

atakapofika shuleni ( Huu siyo miongoni mwa michago ya shule ni huduma ya afya kwaajili ya matibabu kwa mtoto mzazi unapokuwa mbali).

**Kumbuka:-** Fedha ya malipo kwa ajili ya michango mingine ilipwe kwenye Akaunti Namba **51306600111**, katika Benki ya NMB, Jina la Akaunti KALIUA SEC.SCHOOL PROJECT ACCOUNT, ( tafadhali kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay- in slip, kumbuka kuwa hii ni Akaunti kwa ajili ya **MICHANGO MINGINE YA SHULE TU).**

- **Kama hautalipa michango hiyo hapo juu mwanafunzi hata pokelewa kabisa.**

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni:-**

i. Ream ya karatasi moja (**02**) kwa kila muhula wa masomo.
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi aliyochaguliwa kujiunga ( orodha imeambatanishwa).
iii. Dissecting kit, gloves boksi moja na Scientific calculator
iv. Godoro la sponji **6'' x 2.5'' x 4''**
v. Mto mmoja na foronya mbili.
vi. Mkasi wa kukatia maua na miche kwa wanafunzi wa **CBG.**
vii. Shuka mbili rangi ya ***bluu kwa wavulana na rangi ya pinki kwa wasichana*** zisizo na maandishi.
viii. Blanketi moja ***nzito ya rangi ya kijivu*** isiyo na maua na chandarua 1 nyeupe ya pembe nne.
ix. Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
x. Kwanja **01**, jembe **01** lenye mpini, reki **01** yenye mpini**,** blashi ya kusugulia chooni au bafuni yenye mkono mrefu( hardbloom) **02,** na fagio la ndani **02,** squeezer **02** na ndoo **01** ya kuogea.

**TANBIHI**

**Vifaa vifuatavyo vinaweza kupatikana karibu na mazingira ya shule kwani shule ipo mjini patikana.**

1. **Tishirt -Tsh 150000/=**
2. **Sweta -Tsh.15000/=**
3. **Dissecting kit Tsh.30000/=**
4. **Gloves Tsh.10000/=**
5. **Jembe na mpini wake tsh.8000/=**
6. **Kwanja Tsh.4000/=**
7. **Reki na mpini wake tsh.4000/=**
8. **Mfagio mgumu wa chooni Tsh.4000/=**
9. **Mfagio laini na skwiza Tsh.7000/=]**
10. **Ndoo 3000/=**

## 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga nywele ndefu. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au viambatwa vya simu kama laini, betri, chaji ya simu katika mazingira yashule
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xix. Kuruka wigo wa shule au kukamatwa nje ya mipaka ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.

**Aidha**, makosa mengine ambayo hayakutajwa hapo juu, mfano: kukwepa kufanya majaribio, mahudhurio hafifu darasani, kutotii kengele, kutokamilisha kazi za darasani, kutofanya usafi eneo alilopangiwa, kuzungumza Kiswahili ukiwa eneo la shuleni n.k yatatolewa adhabu ndogondogo ndani ya shule ikiwa ni pamoja na adhabu ya kufyatua tofali za kuchoma au kubaki shuleni wakati wa likizo kama ilivyoazimiwa na Bodi ya shule.

- Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya shule kutafuta huduma za kifedha au manunuzi yoyote isipokuwa kwa kusaidiwa na walimu wake walezi wake yaani matron na patron.
- Pia mawasiliano yote ya mwanafunzi na mzazi yatafanyika kupitia kwa mkuu wa shule,makamu mkuu wa shule,patron,na matron
- Taarifa za kuugua au gharama za matibabu za mwanafunzi zitatolea na mkuu wa shule kwa namba zinazoonekana hapo juu.

## 4. Viambatanisho na Fomu Muhimu.

Mwanafunzi ajaze kikamilifu fomu zifuatazo:-

**a)** Fomu ya Uchunguzi wa Afya ( Medical Examination Form)ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. ( **Kiambatanisho ''D''**)

**b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. (**Kiambatanisho ''C''**)

**c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni , kulipa ada na michango mingine na maelekezo mengine yote yatakayotolewa na shule. (**Kiambatanisho ''C''**)

d) Picha nne **(4)** za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu. (**Kiambatanisho ''E''**)

**MUHIMU:-**

1.Shule haitoi mlo maalumu kwa wanafunzi wenye uhitaji wa chakula maalumu, ila kuna sehemu maalum ya kununua chakula ( school canteen)

2. Tarehe ya kufungua na mwisho wa kuripoti hutolewa na Serikali hivyo zingatia tangazo la serikali.

3. Soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.....**

**Ngonile M.Mwasile**

**MKUU WA SHULE**

# KIAMBATISHO 'C'
# FOMU YA KUKUBALI KUANDIKISHWA SHULE

(Ijazwe na kukabidhiwa kwa Msajili wa Wanafunzi siku ya kuripoti shuleni kwa mara ya kwanza)

1. Jina kamili la Mwanafunzi, kama lilivyo katika TSM.9/SEL-FORM (kwa herufi kubwa zote)
   ……..
2. Tarehe ya kuzaliwa……..
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya)……
4. Uraia …….
5. Shule anayotoka ……
6. Dini……..
7. Dhehebu ……
8. Nyumbani: Mkoa…… Wilaya……..
   Kijiji……
9. Jina kamili la Mzazi/Mlezi…….
   Uhusiano na Mlezi kama hana Mzazi ……..
   Anuani ya Mzazi/Mlezi ……..
   Namba ya Simu ya Mzazi/Mlezi (nyumbani)……..
   (Mabadiliko yawasilishwe Ofisini mara moja)……

10. <u>Ahadi ya Mwanafunzi:</u>
    Mimi…….. Ninakubali nafasi ya shule hii niliyopewa. Naahaidi kutii KIKAMILIFU Sheria na Kanuni zote za shule wakati wote niwapo Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kaliua, naahidi kwamba sintashiriki katika migomo, fujo, na makosa mengine ya jinai, na kwamba UTORO KWANGU UTAKUWA NI MWIKO.
    Jina kamili la Mwanafunzi (Majina matatu, likiwamo la mwisho la ukoo).
    ……
11. Misheni (lengo kuu) la Mwanafunzi:
    ……
    …

    Saini ya Mwanafunzi …….
    Tarehe……

12. <u>Ahadi ya Mzazi/Mlezi:</u>
    Nakubali mwanangu …… ajiunge na Shule ya Sekondari Kaliua katika kidato cha …….. mwaka …… na ninaahidi kwamba NITAKUWA NALIPA KARO PAMOJA NA MICHANGO YOTE YA SHULE KWA WAKATI ULIOWEKWA, HADI HAPO ATAKAPOHITIMU KIDATO CHA
    ……..
    Jina kamili la
    Mzazi/Mlezi……..

    Saini ya Mzazi/Mlezi…….
    Tarehe……

**<u>ILANI:</u>**

Mwanafunzi hatasajiliwa kama Fomu hii haitajazwa kikamilifu.

# KIAMBATISHO 'D'
# (To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster Kaliua Secondary School)

NAME:……
……
Please examine the above named student and comment on his/her health by responding to the following items. Kindly put a tick ( V ) in front of either YES or NO whichever applicable:
Does the student have problems in connection with:

1. Sight? …… (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……
2. Hearing? …… (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……
3. T.B.? …… (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……
4. Blood Pressure?..... (a) NO
   (b) YES
   If YES state……..
5. Athma?..... (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……
6. Any other health problems? …… (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……..
7. Any physical disability? …… (a) NO
   (b) YES
   If YES state ……..
8. Do you therefore recommend the said student medically fit for studentship at this School? …… (a) NO
   (b) YES
   If NO please state ……
   ……
   ……..
   ……..

   Name and Signature …….

   ……

   Designation ……

   Date…….. Official Stamp.

## KIAMBATISHO "E"

## UTHIBITISHO WA NDUGU WA MWANAFUNZI

| NA. | PICHA | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

# SHULE YA SEKONDARI KALIUA
# ORODHA YA VITABU VILIVYOPO

1. **BIOLOGY**
   (a) Understanding to biology Advanced biology
   (b) Tanzania Institute of Education Biology form V and VI
   (c) Chand Biology
   (d) Tanzania institute of Education biology form one and two.
   (e) Understanding biology form 3 and 4
2. **CHEMISTRY**
   (a) Chemistry for Secondary Schools form V and VI (TIE)
   (b) Understanding Chemistry by Ted-lister
   (c) Ramsden EN(2000) Advanced level Chemistry 4th edition United Kingdom
   (d) Inorganic Chemistry part A Mzumbe book project
   (e) Understanding Chemistry for Advanced level (3rd edition 2000) Nelson Thornes
   (f) East Africa chemistry for o-level.
   (g) Tanzania institute of education chemistry form one ,two,three and four.
3. **GEOGRAPHY**
   (a) Principles of Physical geography by Francis J. Monkhonse (1975)
   (b) Research Methodology by C.R. Kothani
   (c) Practical Geography for Africa by J.M. Pritchard (1984)
   (d) DT Msabila (2009) Physical Geography for Advanced level
   (e) Elementary Physical Geography (2013) by Ahmed Lubwana
   (f) R.B. Bunnet (1984) Physical Geography in Diagrams for Africa
   (g) David Waugh (2002) Geography An Integrated Approach 3rd Edition
   (h) T.I.E geography for o-level

4. **PHYSICS**
   (a) Principles of Physics Class XI and XII by S. Chands
   (b) Advanced Physics by Michael Nelkon
   (c) Fundamental of Physics by Resnick
   (d) University Physics
   (e) Understanding Physics
   (f) Advanced Physics (Roger Muncaster)
   (g) Physics for ordinary level
   (h) Understanding physics form 1-iv.
5. **BASIC AND APPLIED MATHEMATICS**
   (a) BAM for advanced level , Respicius Kiiza, Lugano Mwangide (Nyambari Nyangwine)(2008)
   (b) BAM for Advanced Secondary Schools form V and V by Septone/Sollem Published by GDY (2014)
   (c) BAM for Advanced Secondary Schools form Five and Six by TIE (2006)
   (d) T.I.E Basic mathematics for ordinary level.
6. **ADVANCED MATHEMATICS**
   (a) S. Chand's for Class xi and xii
   (b) Pure Mathematics 1 and 2

(c) Advanced Mathematics Tranter
(d) Understanding Mathematics

7. **G.S.**

(a) CETA, G.S Advanced level
(b)Mbalase, F.R (2011). General Studies Advanced level 5 and
c) Fundamental of civics for ordinary level.
d) Civics for secondary schools .